**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**WIZARA YA KAZI NA UWEKEZAJI**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA KAZI NA UWEKEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**ILIYOWASILISHWA NA**
**MHESHIMIWA SHARIFF ALI SHARIFF (MBM)**
**KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR**

**ZANZIBAR** **MEI 2026**



**MHESHIMIWA SHARIFF ALI SHARIFF (MBM)**

**WAZIRI WA KAZI NA UWEKEZAJI**
**ZANZIBAR**

## YALIYOMO


YALIYOMO .......... i
VIFUPISHO VYA MANENO .......... ii
**A. UTANGULIZI** .......... 1
**B. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI ZAKE** .......... 4
**C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MSINGI YA WIZARA** .......... 5
i. Mapato yaliyokusanywa na Wizara ikilinganishwa na malengo yaliyowekwa .......... 6
ii. Matumizi ya Wizara ikilinganishwa na Malengo .......... 6
iii Mafanikio na changamoto za Wizara .......... 7
iv Utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha Julai, 2025 - Machi 2026 .......... 9
Programu Kuu P01 : Uendeshaji na Uratibu wa Wizara .......... 9
Programu Kuu P02: Usimamizi wa Sheria za Kazi na Upatikanaji wa Ajira .......... 10
Programu Kuu P03: Programu Kuu ya Kukuza na Kuimarisha Uwekezaji Nchini .......... 10
v) Utekelezaji wa Vipaumbele kwa Mujibu wa Mpango Mkakati wa Wizara na Taasisi .......... 10
Programu Kuu: Uendeshaji na Uratibu wa Wizara .......... 10
Programu Kuu: Usimamizi wa Sheria za Kazi na Upatikanaji wa Ajira .......... 13
Programu Kuu: Kukuza na Kuimarisha Uwekezaji Nchini .......... 17
**D. UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA JULAI 2025 - MACHI 2026** .......... 18
**E. MWELEKEO WA UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE VYA MATUMIZI KWA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027** .......... 20
i Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) .......... 21
ii Kampuni ya Uwekezaji ya Zanzibar ( Zanzibar Investment Company Limited) .......... 21

**F. MWELEKEO WA VIPAUMBELE VYA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027** ........ 23
i Program za Wizara ya Kazi na Uwekezaji ........ 23
Programu Kuu: Uendeshaji na Uratibu Wa Wizara ........ 23
Programu Kuu: Usimamizi wa Sheria za Kazi na Upatikanaji wa Ajira ........ 24
Programu Kuu: Kukuza na Kuimarisha Uwekezaji Nchini ........ 26
ii Uzingatiaji Usawa wa Kijinsia ........ 27
ii Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ........ 28
**SHUKURANI NA HITIMISHO** ........ 29
**G. VIAMBATISHO** ........ 34

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| AFCON | African Cup of Nations |
| AfDBA | African Development Bank |
| ATE | Association of Tanzania Employers |
| BAMAS | Bajeti ya Mapinduzi Serikalini |
| CCTV | Closed Circuit Television |
| EAC | East African Community |
| ILO | International Labour Organisation |
| IOM | International Organisation for Migration |
| MTEF | Mid Term Expenditure Framework |
| OCGS | Office of Chief Government Statistic |
| PBZ | Peoples' Bank of Zanzibar |
| PCF | Private Capital Flows |
| PDF | Project Development Fund |
| PPP | Public Private Partnership |
| SEZs | Special Economic Zones |
| SJMT | Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| SNR | Sema na Rais Mwinyi |
| SP | Strategic Plan |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TZS | Tanzania Shillings |
| UAE | United Arab Emirates |
| UNDP | United Nation Development Programmes |
| USD | United State Dollar |
| WB | World Bank |
| ZAA | Zanzibar Airport Authority |
| ZADEP | Zanzibar Development Plan |
| ZANEMA | Zanzibar National Employment Association |
| ZATUC | Zanzibar Trade Union Congress |
| ZICL | Zanzibar Investment Company Limited |
| ZIEW | Zanzibar Investment Electronic Window |
| ZIPA | Zanzibar Investment Promotion Authority |
| ZSSF | Zanzibar Social Security Fund |
| ZPDB | Zanzibar Presidential Delivery Bureau |

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Naomba nianze hotuba yangu kwa Kumshukuru Allah (Subhanahu Wataala) kwa Rehma zake na kutujaalia uhai, uzima wa afya, amani na utulivu katika Nchi yetu na kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

2. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza hili lipokee, lijadili na hatimae liidhinishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

3. **Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima kubwa naomba kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati ya moyo wangu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika awamu ya sita (6) na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa kwa mara nyengine tena kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Awamu ya nane (8) katika Kipindi cha Pili. Katika kipindi cha uongozi wao, Serikali zote mbili zimeendelea kusisitiza amani na utulivu, uchumi shindani, diplomasia ya uchumi na mazingira rafiki kwa biashara na uwekezaji, sambamba na kuimarisha uwajibikaji na usimamizi wa rasilimali za Umma. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa Afya Njema, Uwezo na Busara ya kuliongoza na kulitumikia Taifa letu.

4. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, nachukua fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mafanikio makubwa aliyoyapata katika kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa mwaka 2021-2026. Katika uongozi wake wananchi wa Zanzibar tumeshuhudia kuimarika kwa Uchumi, Huduma za kijamii na maendeleo kupitia Sekta za Utalii, Uchumi wa Buluu, Elimu, Afya, Miundombinu, na Biashara. Mafanikio yaliyopatikana katika Sekta za Kazi na Uwekezaji ni pamoja na kuzalisha nafasi mpya za kazi 233,615, Usajili wa Miradi 606 kupitia

ZIPA ikiwemo Miradi 15 ya Visiwa vidogo vidogo, Usajili wa Miradi 26 kupitia Ushirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) na Uanzishwaji wa Kampuni ya Uwekezaji inayomilikiwa na Serikali.

5. **Mheshimiwa Spika,** Nampongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kufuatilia kwa karibu utendaji wa Serikali ikiwemo Wizara yangu kupitia maagizo, maelekezo yake ya moja kwa moja na kupitia Taasisi ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Mheshimiwa Rais (ZPDB) pamoja na Mfumo wa Sema na Rais Mwinyi (SNR).Utaratibu huo umeimarisha ufanisi katika Utendaji,Uwajibikaji na Usimamizi wa Majukumu ya Wizara yangu, katika kuimarisha huduma na kutatua changamoto zinazowakabili Wananchi, Wafanyakazi, Waajiri na Wawekezaji katika Sekta yangu.

6. **Mheshimiwa Spika**, Namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kukubali kuwa Mgeni Rasmi katika Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani - Mei Mosi licha ya majukumu mengi aliyonayo. Uwepo wake katika Maadhimisho hayo kila mwaka ni ushahidi tosha wa kuthamini Wafanyakazi na mchango wao katika Ustawi wa Zanzibar, ambapo katika maadhimisho ya mwaka huu 2026 yaliyofanyika Dole, Mkoa wa Mjin Magharibi amepandisha kima cha chini cha Mshahara kutoka TZS 300,000 hadi kufikia TZS 500,000 sawa na Asilimia 60.

7. **Mheshimiwa Spika,** Nawapongeza Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla Makamu wa Pili wa Rais, Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri pamoja na Mheshimiwa *Balozi Mhandisi* Zena Ahmed Said aliyekuwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi kwa kumshauri na kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza Mipango ya Serikali na kutimiza azma na malengo yake ya kuiletea maendeleo Zanzibar na wananchi wake.

8. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, napenda kuwapongeza na kuwashukuru Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kwa mara nyengine, na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuchaguliwa kwa mara ya kwanza, kuliongoza Baraza

la Wawakilishi. Pia, nawashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Wenyeviti wa Baraza kwa kuendesha vikao vya Baraza la Wawakilishi kwa umahiri na uweledi mkubwa. Kipekee, namshukuru Mheshimiwa Makame Mohammed Sufiyani kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mahmoud Omar Hamad kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Uwekezaji ya Baraza hili na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati pamoja na Makatibu wa Kamati hiyo kwa mashirikiano makubwa wanayotupatia katika kufanikisha utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2025/2026 na kufanya mapitio ya Bajeti hii ya mwaka 2026/2027. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako kwa ushauri, maelekezo na michango yao wanayonipatia ambayo yamefanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

9. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya utangulizi, salamu na pongezi, naomba uniruhusu kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ikijumuisha Vipaumbele vya Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara, Utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Wizara (Ukusanyaji wa mapato, Mafanikio na Changamoto, Utekelezaji wa Programu Kuu na Ndogo na Utekelezaji wa Vipaumbele kwa mujibu wa Mpango Mkakati wa Wizara na Taasisi zake). Hotuba hii pia inajumuisha Utekelezaji wa Bajeti za Taasisi kwa Julai 2025-Machi 2026 na Mwelekeo wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Matumizi kwa Taasisi zinazosimamiwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Mwelekeo wa Vipaumbele vya Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027 na Viambatisho husika.

## B. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI ZAKE

8. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara imepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

1. Kusimamia utekelezaji wa Sheria, viwango vya kazi, kazi za staha, mahusiano kazini, ulinzi wa haki za wafanyakazi na utatuzi wa migogoro ya kazi na kuboresha kima cha chini cha mishahara.
2. Kusimamia Usalama na Afya za Wafanyakazi wakiwa Kazini kupitia mifumo kinga ya Kuzuia ajali kazini, Magonjwa yanayotokana na kazi na kuimarisha uzingatiaji na udhibiti wa vihatarishi sehemu za kazi.
3. Kukuza na kuwezesha Uwekezaji Binafsi kwa kuimarisha mazingira ya uwekezaji, mifumo rafiki ya Tehama, miundombinu ya uwekezaji katika maeneo huru, na kurahisisha taratibu za utoaji huduma (One-Stop Center) ili kushajihisha uwekezaji wenye tija zaidi wa kimkakati na uwekezaji katika visiwa vidogo vidogo.
4. Kuratibu uwekezaji wa umma kupitia mfumo wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) kwa mujibu wa Sheria ya PPP ya Zanzibar, katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya miundombinu na huduma za kijamii pamoja na kiuchumi, ikiwemo sekta ya usafirishaji na miundombinu, nishati na umeme jadidifu, maji na usafi wa mazingira, Afya, Elimu, TEHAMA na Uchumi wa Kidijitali, Uchumi wa Buluu, Utalii, Biashara na Masoko, pamoja na Sekta nyengine zinazochochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi.
5. Kusimamia na kuratibu uandaaji na utekelezaji wa Mipango, Sera Tafiti na usimamizi wa Rasilimali Watu na Fedha pamoja na kukamilisha mchakato wa kuhuisha muundo wa Kamisheni ya Kazi, Kitengo cha Usuluhishi na uamuzi wa Migogoro ya Kazi na Idara ya Usalama na Afya Kazini, kuwa taasisi na Idara zinazojitegemea kuendana na ongezeko la mahitaji ya huduma na malengo mapya.
6. Kufanya mapitio ya viwango vya mishahara katika sekta binafsi na kutangaza rasmi, kima cha chini cha mshahara kwa Sekta Binafsi kwa kuzingatia matokeo ya tathmini ya viwango vya mshahara iliyofanyika mwaka 2026.

## C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MSINGI YA WIZARA

9. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kazi na Uwekezaji imeanzishwa kwa mujibu wa Tamko la Kisheria (Legal Notice) Namba 154 mwezi Disemba 2025. Wizara hii inaundwa na Idara tano (5), Taasisi moja (1), Kampuni moja (1) na Ofisi Kuu Pemba. Lengo kuu la kuanzishwa Wizara hii ni kusimamia masuala ya Kazi na Uwekezaji kwa kutekeleza majukumu ya msingi yafuatayo:-

    i. Kusimamia masuala ya Kazi katika Sekta Binafsi.
    ii. Kukuza mashirikiano mazuri kati ya Taasisi za kazi za Kitaifa na Kimataifa.
    iii. Kuhakikisha na kuhamasisha Mahusiano mazuri ya kazi (na kupunguza migogoro ya kazi) kati ya Serikali, Waajiri na Vyama vya Wafanyakazi.
    iv. Kusimamia utekelezaji wa Mikataba ya Kazi ya Kimataifa.
    v. Kusimamia Viwango vya Usalama na Afya katika sehemu za Kazi
    vi. Kuhakikisha utii wa Sheria zinazohusiana na Kazi katika sehemu za Kazi kwa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.
    vii. Kukuza na kusimamia Uwekezaji Nchini.
    viii. Kusimamia shughuli za Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar
    ix. Kukuza uwekezaji wa miradi kupitia Ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (Public Private Partnership).
    x. Kusimamia shughuli za Kampuni ya Uwekezaji ya Serikali (Government Investment Company Limited).
    xi. Kupokea malalamiko kutoka kwa jamii na kuyafanyia kazi ipasavyo
    xii. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Sekta za Kazi na Uwekezaji.
    xiii. Kufanya na kuhamasisha utafiti unaohusiana na maendeleo ya sekta za Kazi na Uwekezaji.
    xiv. Kusimamia Rasilimali watu, fedha na rasilmali nyenginezo.

i. **Mapato Yaliyokusanywa na Wizara Ikilinganishwa na Malengo Yaliyowekwa.**

10. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ilikadiriwa kukusanya Mapato ya TZS. 7,209,087,725. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026 imekusanya Jumla ya TZS. 4,819,133,207 sawa na asilimia 94 kwa makadirio ya miezi tisa ya TZS. 5,125,124,293 na asilimia 67 kwa makadirio ya mwaka ya TZS 7,209,087,725. **Kiambatisho namba 1 kinafafanua.** Hadi kufikia Juni 2026, Wizara inatarajia kukusanya Jumla ya TZS. 7,353,000,000 sawa na asilimia 102 ya makadirio ya mwaka, kutokana na kuengezeka kwa utoaji wa vibali , Uthibitishaji wa Mikataba na Usajili wa maeneo ya kazi na kuanza matumizi ya mfumo wa kieletroniki.

ii **Matumizi ya Wizara Ikilinganishwa na Malengo**

11. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji iliidhinishiwa Jumla ya Matumizi ya TZS 42,456,800,000 ambapo kwa Fungu la A07 lililosimamiwa na Wizara, lilipangiwa Jumla ya TZS 28,700,300,000 na Fungu la A11 lililosimamiwa na Wakala wa Uwezeshaji (ZEEA) lilipangiwa 14,656,600,000. Katika Fungu A07, mishahara ni TZS 7,815,700,000, matumizi ya kawaida TZS 5,884,600,000 na Miradi ya Maendeleo TZS 15,000,000,000. Katika Fungu A11 mishahara ni TZS 1,733,400,000, matumizi ya kawaida TZS. 2,323,200,000 na Miradi ya Maendeleo TZS 10,600,000,000.

12. **Mheshimiwa Spika,** Mnamo mwezi Novemba 2025 Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alifanya mabadiliko ya Muundo wa Wizara za Serikali ambapo kwa Wizara yangu, Wakala wa Uwezeshaji (Fungu A11) na Idara ya Maendeleo ya Ushirika pamoja na Idara ya Ajira ya Fungu (A07), na zimehamishiwa katika Wizara Mpya ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji. Kutokana na mabadiliko hayo, jina la Wizara lilibadilika kutoka Ofisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji na kuwa Wizara ya Kazi na Uwekezaji na hivyo Wizara ilibakiwa na Jumla ya TZS 27,750,285,000 ambapo mishahara ni TZS 7,509,457,000 matumizi ya kawaida TZS 5,240,828,000 na Miradi ya Maendeleo TZS 15,000,000,000

13. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai – Machi, 2025/2026, Wizara imeingiziwa Jumla ya TZS 10,081,077,681 sawa na asilimia 36 ya makadirio ya mwaka TZS 27,750,285,000 na sawa na asilimia 48 ya makadirio ya miezi tisa ya TZS 20,879,798,806. Kati ya TZS 10,081,077,681 zilizoingizwa, mishahara ni TZS 5,222,883,882 sawa na asilimia 93 ya makadirio ya mwaka ya TZS 7,509,457,000, Matumizi ya Kawaida TZS 1,327,680,394 sawa na asilimia 33 ya makadirio ya mwaka ya TZS 5,240,828,000 na Mradi wa Maendeleo wa Uimarishaji wa Maeneo Huru ya Uchumi kwa ujenzi wa barabara TZS 3,468,642,861 sawa na asilimia 23 ya makadirio ya mwaka ya 15,000,000,000. **Kiambatisho namba 2a kinafafanua uingiaji wa fedha kwa kila programu.**

**iii. Mafanikio na Changamoto za Wizara**

14. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara imepata mafanikio yafuatayo:

1. Kukamilisha Mfumo wa kidigitali wa usimamizi wa taarifa za masuala ya kazi (E- Labour Management System) kwa lengo la kuwezesha kufanya kazi kwa njia ya mtandao (online services) na hivyo, kuongeza kasi ya utoaji wa huduma bora.
2. Kuratibu vikao vya kila robo mwaka vya Wadau wa masuala ya Kazi kutoka ZATUC, ZANEMA na Taasisi za Serikali ili kutatua changamoto za masuala ya kazi, ambapo hadi April 2026 jumla changamoto 24 kati ya Changamoto 29 zilizopokelewa na kujadiliwa, zimepatiwa ufumbuzi.
3. Kukamilisha na kuzindua Mpango wa Nchi wa Kazi za Staha wa III *(Decent Work Country Program III 2026/2030)* kwa ajili ya kukuza fursa za kazi zenye tija, usawa, usalama na utu kwa jinsia zote kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Mahusiano, ZATUC, TUCTA, ATE, ZANEMA na ILO.
4. Kuzindua Kitabu cha Taarifa za Uwekezaji kinachoonyesha mwenendo wa Uwekezaji nchini kwa mwaka 2024, ambacho kitatolewa kila mwaka, sambamba na kuzindua Jarida Maalum linaloonyesha Utekelezaji wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa miradi yote ya Uwekezaji katika Sekta zote, kwa kipindi cha Miaka 5, Jarida litakalotumika kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo Zanzibar pamoja na kuonesha utayari wa Serikali katika kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini kwa kujenga miundombinu muhimu tayari kwa Uwekezaji.

5. Kuanza Ujenzi wa Miundombinu ya barabara ya Kilomita 8 katika Maeneo Huru ya Uchumi Fumba kwa lengo la kulihifadhi Maeneo hayo.

6. Kuzindua Miradi 17 ya Uwekezaji yenye mitaji wa thamani ya USD 243.8 milioni na kutoa ajira zaidi ya 1,567. Miongoni mwa miradi hio ni Mradi wa Kiwanda na Shamba la Kuku la ZANBREED CHICKEN FARM uliopo Kitope wenye mtaji wa USD 105 milioni na kutoa ajira zipatazo 1,000, Mradi ambao ulizinduliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Mradi mwengine ni Hoteli ya JAZ ELITE AURORA uliopo Michamvi wenye mtaji wa USD 100 milioni na kutoa ajira zipatazo 200, Mradi ambao ulizinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan

7. Kuratibu Miradi 6 ya Ushirikiano baina Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) yenye thamani ya TZS. Bilioni 752,730,739,800 katika Usimamizi na Uendeshaji wa Viwanja vya Michezo 17 katika Wilaya na Mikoa;Ujenzi na Uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege kilichopo Kigunda Nungwi; Ukarabati , Uendeshaji na Usimamizi wa Maeneo ya kihistoria,Ujenzi na Uendeshaji wa Bustani ya Africa House Ujenzi, Uendeshaji na Usimamizi wa Kituo cha Ukaguzi wa Vyombo vya Moto Dole na uendeshaji na usimamizi wa Bohari ya Mafuta Mangapwani. Uwekezaji huu unafikisha jumla ya Miradi ya PPP 26 yenye thamani USD 1.2 Bilioni

8. Uanzishwaji wa Kampuni ya Uwekezaji inayomilikiwa na Serikali kwa lengo la kuongeza wigo kwa wawekezaji ambao wanania ya kuwekeza kwa utaratibu wa hisa kwa kushirikiana na Serikali.

15. **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mafanikio hayo, kulikua na changamoto zifuatazo;

1. Kutokamilika kwa miradi ya maendeleo katika maeneo huru ya uchumi kwa wakati na kutofikia malengo ya utekelezaji wa mujukumu ya Wizara unaosababishwa na upatikanaji mdogo wa fedha.
2. Uchambuzi wa vyanzo vya mapato kutokana na kasma tofauti unaopelekea ukadiriaji usio sahihi wa ukusanyaji wa mapato.

16. **Mheshimiwa Spika,** Wizara itachukua hatua zifuatazo katika kutatua changamoto hizo;

1. Wizara inaratibu ufuatiliaji wa fedha kwa kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuomba kuingiziwa fedha kwa mujibu wa mpango kazi.

2 Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango inaratibu uchambuzi wa vyanzo vya mapato kutokana na kasma tofauti kwa Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar, Kamisheni ya Kazi, Idara ya Usalama na Afya Kazini na Kitengo cha Usuluhishi wa Migogoro.

**iv Utekelezaji wa Programu Kuu na Programu Ndogo Ikijumuisha Fedha za Miradi ya Maendeleo na Matumizi ya kawaida kwa kipindi cha Julai, 2025 - Machi 2026**

17. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ina Programu Kuu Tatu (3) na Programu Ndogo Ndogo Saba (7). **Kiambatisho namba 3 kinafafanua.**

**Programu Kuu P01: Uendeshaji na Uratibu wa Wizara**

18. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina Programu Ndogo Tatu ambazo ni Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti, Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji na Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara katika ofisi kuu Pemba. Programu hii ilikadiriwa Matumizi ya TZS. 4,574,610,359 hadi kufikia Machi, 2026 imepatiwa TZS. 2,897,282,394 sawa na asilimia 63 ya makadirio.

**Programu Kuu P02: Usimamizi wa Sheria za Kazi na Upatikanaji wa Ajira.**

19. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina Programu Ndogo Mbili ambazo ni Programu ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini na Programu ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi na Usuluhishi wa Migogogro ya Kazi. Programu hii ilikadiriwa Matumizi ya TZS. 1,586,039,197 hadi kufikia Machi, 2026 imepatiwa TZS. 958,504,421 sawa na asilimia 60 ya makadirio.

**Programu Kuu P03: Programu Kuu ya Kukuza na Kuimarisha Uwekezaji Nchini.**

20. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina Programu Ndogo mbili ambazo ni Programu ya Usimamizi wa Uwekezaji Binafsi na Programu ya Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma kupitia UshirikianoUshirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP). Programu hii iliidhinishiwa Matumizi ya TZS. 14,719,149,250 hadi kufikia Machi, 2026 imepatiwa TZS. 6,225,290,866 sawa na asilimia 42 ya makadirio.

**v) Utekelezaji wa Vipaumbele kwa Mujibu wa Mpango Mkakati wa Wizara na Taasisi**

**Programu Kuu: Uendeshaji na Uratibu wa Wizara.**

21. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026, imetekeleza shughuli zifuatazo;

    1. Imeandaa Mpango Mkakati kwa lengo la kuweka dira na malengo na vipaumbele vya Wizara, kuimarisha matumizi ya rasilimali (fedha na watu), kupima utendaji na kukabiliana na changamoto zilizopo
    2. imeandaa Mpango Mkakati wa Takwimu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa takwimu kiurahisi na kuratibu takwimu za kiutawala za Wizara.
    3. Imeandaa ajenda ya Utafiti katika maeneo ya Kazi, Uwekezaji, Utatuzi wa Migogoro ya Kazi, Afya na Usalama Kazini, Uendeshaji na Mipango.
    4. Imeimarisha Ufuatiliaji na Tathmini kwa kujenga uwezo wa watendaji.

5. Imefanya mikutano ya Uratibu wa utekelezaji wa Sera za Wizara kwa Unguja na Pemba kwa lengo la kutoa nafasi kwa wadau kutoka Sekta za Serikali na Sekta Binafsi kutoa maoni na mapendekezo kuhusu Sera zinazohusiana na Wizara.

6. Imeshiriki mikutano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ikiwemo mashirikiano ya Mawizara kati ya SJMT na SMZ, maeneo ya kazi na uwekezaji ya Jumuiya ya EAC kwa lengo la kuimarisha ukuaji wa masuala ya sekta ya Kazi na Uwekezaji.

7. Imeimarisha utendaji wa wafanyakazi 32 (Wanawake 20 na Wanaume 12) kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi yanayohusu Ufuatiliaji na Tathmini, Mashirikiano baina ya sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sheria na kanuni za Utumishi, ukaguzi wa ndani, uendeshaji na usimamizi wa miradi, ufanisi na weledi wa masekretari, uhariri wa picha, mfumo wa BAMAS, matayarisho ya kustaafu, na wafanyakazi 16 (Wanawake 9 na Wanaume 7) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu yanahusu TEHAMA, Rasilimali Watu, Uongozi wa Biashara, Habari na Mawasiliano, Uhasibu, Uchumi na Fedha, Maendeleo ya Sera, Uendeshaji wa Biashara na Miradi na Manunuzi

8. Imeendelea kutumia mifumo ya Ofisi ikiwemo E – Office, Assets Register, na mfumo wa usimamizi wa Rasilimali watu (Human Resources Management) kwa kuweka taarifa na kupatikana huduma.

9. Imesimamia maslahi na stahiki za watumishi ikiwemo likizo, ubani na posho pamoja na ushirikiano mzuri kati ya viongozi na wafanyakazi kupitia vikao vya Kamati Tendaji na Kamati ya Uongozi

10. Imeimarisha mazingira ya miundombinu ya Wizara kwa kuweka Lami katika eneo la ndani na nje kwa ufadhili na ushirikiano wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

22. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara katika Ofisi Kuu Pemba imetekeleza yafuatayo:-

1. Imesimamia maslahi ya wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi Sita (6) Wanawake watatu (3) na Wanaume watatu (3) katika fani ya utunzaji wa kumbukumbu na ukaguzi wa ndani (Internal Audit), uhasibu na uandishi wa habari.

2. Imefanya malipo ya safari za ndani ya Nchi kwa ajili ya kushiriki katika vikao na shughuli zinazohusiana na Kamati ya Uongozi, Kamati Tendaji, Kamati ya Uchumi na Uwekezaji na masuala ya mashirikiano kwa Unguja na Tanzania Bara. Aidha, imelipa posho ya likizo kwa wafanyakazi watatu (3) wakiwemo Mwanamke mmoja (1) na Wanaume wawili (2), posho la masaa ya ziada (over time), posho la ubani kwa mfanyakazi mmoja (1) pamoja na kufuatilia malimbikizo ya posho mbali mbali.

3. Imefanya zoezi la uhakiki na marekebisho ya mfumo wa Rasilimali watu pamoja na mfumo wa malipo, sambamba na kufanya mnada wa uuzaji wa vifaa chakavu.

4. Imetoa mafunzo kwa wafanyakazi wapya wanane (8), wakiwemo wanawake watano (5) na Wanaume watatu (3),kuhusu umuhimu wa maadili katika sehemu za kazi pamoja na haki na fursa za watumishi kazini. Mafunzo haya yametolewa kwa lengo la kujenga msingi imara wa maadili mema katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

5. Imeratibu na kufanya vikao vitano (5) na watendaji kwa lengo la kujadili mipango na mikakati ya utekelezaji wa majukumu ya Idara ili kufikia malengo yaliyopangwa, licha ya changamoto zilizopo zikiwemo uhaba wa watendaji, usafiri na uingizwaji mdogo wa fedha za matumizi ya kawaida.

6. Imefanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya hoteli, viwanda pamoja na Mradi wa Ufugaji nyuki uliolenga kuanzisha warsha ya utengenezaji wa Mizinga na vifaa vya Pollen Traps,pamoja na kuanzisha Shamba darasa la ufugaji wa Nyuki katika eneo la kituo. Hatua hiyo imelenga

kuongeza kasi ya utoaji wa mafunzo kwa vitendo na kuongeza ufanisi wa shughuli za ufugaji wa Nyuki.

7. Inaendelea kuielimisha jamii kupitia Vyombo vya Habari nchini, ikiwemo Redio, Televisheni, Magazeti, na mitandao ya kijamii, kuhusu utekelezaji wa shughuli za Wizara. Katika kipindi hicho, habari 20 zimeandaliwa na kurushwa hewani, vipindi vinne (4) vimerushwa kupitia Redio na Televisheni, na Makala kumi na moja (11) zimeandaliwa katika Gazeti la Zanzibar Leo. Aidha, inaendelea kutatua changamoto zinazoripotiwa kupitia mfumo wa Sema na Rais Mwinyi (SNR). Vilevile, imewapatia mafunzo watendaji 30 kuhusu Afya ya akili na matumizi ya Takwimu kupitia mfumo wa SPSS na

8. Imeandaa dhana ya mradi kuhusu ajira za watoto wenye mada "From hazardous work to safe learning: Eliminating child labour among vulnerable children in Pemba Region." Dhana hiyo imewasilishwa kwa wadau mbalimbali ili kupata ufadhili wa utekelezaji katika mwaka wa bajeti 2026/2027. Kupatikana kwa ufadhili kutaiwezesha Wizara kuwaondoa watoto 400 kila mwaka kutoka ajira hatarishi kwa kipindi cha miaka mitatu (3), kurejesha watoto 300 skuli, na kuwapatia watoto 100 mitaji ya kujikimu.

**Programu Kuu: Usimamizi wa Viwango vya Kazi na Upatikanaji wa Ajira**

**23. Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026, imetekeleza shughuli zifuatazo;

1. Imefanya ukaguzi kazi wa kawaida kwa Taasisi 326 (Unguja 240 na Pemba 96) kwa lengo la kuhakikisha Taasisi hizo zinatekeleza Sheria za kazi katika kulinda haki na Maslahi ya wafanyakazi.

2. Imefanya ukaguzi kazi maalum kwa Taasisi 11 ili kuangalia uwezo wa ulipaji wa kima cha chini cha mshahara ambapo Taasisi 9 zilipatiwa cheti maalum baada ya Kamisheni kujiridhisha kuwa taasisi hizo zimekidhi sifa na vigezo vya kulipa kima cha chini cha mishahara cha TZS. 347,000. Taasisi 2 zinaendelea kufanyiwa uhakiki na ukaguzi. Taasisi zilizokaguliwa ni pamoja na Skuli binafsi, Kampuni za Ulinzi, Kampuni za Ujenzi, Kampuni za usafi na Mikahawa.

3. Imethibitisha jumla ya mikataba ya wafanyakazi 11,613 (Unguja 9,790 na Pemba 1,823) Wanaume 7,592 na Wanawake 4,021 sawa na asilimia 111 ya makadirio ya 10,500 kwa lengo la kuhakikisha masharti na viwango vya Mikataba hiyo vinaendana na Sheria, Kanuni na Miongozo ya kazi iliopo Nchini.

4. Imetoa Vibali vya Kazi kwa wageni 2,877 kutoka katika Mataifa mbalimbali yakiwemo ya Italia, Ujerumani, Marekani, Uingereza, Uturuki, Ethiopia, India, China, Korea na Afrika ya Kusini, Waliopatiwa vibali vya msamaha wa Mheshimiwa Waziri ni 169, waliopatiwa vya msamaha kwa miradi iliyoidhinishwa ZIPA ni 169, vibali vipya ni 1,248, vibali vilivyoongezwa muda ni 731, vibali vya muda mfupi ni 540 pamoja na Diaspora 20.

5. Imeratibu usimamizi wa viwango vya kazi vya mikataba ya wafanyakazi 1,807 (wanawake 1,531 na wanaume 276) waliopata kazi nje ya nchi wakiwemo waliosafirishwa kwenda Oman, Qatar na U.A.E.

6. Imeendelea kupambana na Tatizo la utumikishwaji wa Watoto katika sehemu za kazi ambapo Watoto 778 waliingia kutoka Tanzania Bara na Watoto 30 wameondolewa katika maeneo ya kazi.

7. Imepokea migogoro ya kazi 295, ambapo migogoro 113 imesuluhishwa, migogoro 171 bado inaendelea na hatua za usuluhishi, na migogoro 11 imefutwa baada ya walalamikaji kushindwa kufuatilia madai yao. Kwa ambao hawakuridhika na uamuzi huo au kutokutekeleza hukumu Mashauri yanawasilishwa katika Mahakama ya Kazi kwa hatua.

8. Inaendelea na hatua za kuridhia mikataba sita ya Shirika la Kazi Duniani kwa kuwasilishwa Serikalini. Mikataba hiyo ni Hifadhi ya Jamii, Mafao ya Wafanyakazi wanaopata majanga kazini, Wafanyakazi wa majumbani, Sera ya Ajira, Usalama wa Afya na Kazini na Mfumo wa Uhamasishaji wa masuala ya Usalama na Afya katika sehemu za Kazi.

9. Imekamilisha mchakato wa kufanya tathmini ya viwango vya mshahara kwa Sekta Binafsi, iliyozingatia vigezo mahsusi vikiwemo Hali ya Uchumi, Gharama za Maisha, Mfumko wa Bei, Hali ya Soko la Ajira, Uwezo wa waajiri na Taasisi Kiuchumi pamoja na Tija na ufanisi wa mfanyakazi.

10. Imehakiki na kufanya ukaguzi maalum kwa wafanyakazi 532 waliopoteza ajira ambapo jumla ya wafanyakazi 531 (wanaume 378 na wanawake 153) wamewasilishwa ZSSF kwa hatua stahiki za malipo ya fao la upotevu wa ajira na mfanyakazi 1 hakuthibitika kwa kutokidhi vigezo vilivyowekwa.

11. Imeimarisha mashirikiano ya UTATU kwa kusimamia malalamiko ya wafanyakazi wa chama cha ZAFICOWU na ZETHAU waliokuwa wakilalamika kutolipwa kwa ada ya uanachama pamoja na malipo ya fedha kutoka kwa mwajiri husika na tayari imeshalipwa.

12. Imetoa elimu kazi kwa Taasisi 41 (20 Unguja na 21 Pemba) kwa waajiri, wafanyakazi na jamii kwa ujumla juu ya taratibu za Sheria, Kanuni, Miongozo, haki na wajibu wa masuala ya Kazi pamoja na utoaji wa huduma ya kwanza kazini. Elimu hiyo imetolewa katika sehemu za Kazi na kupitia vyombo vya Habari (TV na Redio). Aidha, imewapatia elimu juu ya athari za Ajira za Watoto kwa Masheha 112 (Wilaya ya Mjini 39, Wilaya ya Kati 33, Wilaya ya Kaskazini A 40)

13. Imefanya ukaguzi sehemu za kazi 365 (Unguja 271, Pemba 94) ambazo zimepewa miongozo kwa waajiri na waajiriwa juu ya umuhimu wa Usalama na Afya Kazini ambapo asilimia 75 ya Taasisi hizo zimeonekana zimekidhi vigezo na asilimia 25 zimeonekana na mapungufu yakiwemo vihatarishi (occupational harzard) vinavyohusiana na Mfumo kinga wa vifaa vya kujikinga na ajali za moto pamoja na mazingira ya usafi wa sehemu za kazi.

14. Imefanya uchunguzi wa Ajali 7 za moto (5 Unguja, 2 Pemba) ziliripotiwa ambazo ni skuli 2, hoteli 2, Kituo cha kujazia mafuta 1, Matengenezo ya Umeme 1 na bekari 1, wafanyakazi 4 wamefariki kwa ajali ya moto; Ajali 9 za ujenzi (8 Unguja, 1 Pemba) ziliripotiwa

ambazo wafanyakazi 8 walipoteza viungo (3 macho, 1 mkono, 1 mguu na 3 vidole) na 1 alifariki dunia; Ajali 1 ya barabarani imeripotiwa Pemba ambapo mfanyakazi 1 alifariki dunia.

15. Imefanya usajili wa sehemu za kazi 168 (Unguja 129, Pemba 39) kwa lengo la kuzitambua zipo katika maeneo gani na zinafanya shughuli gani ili ziweze kufikiwa kwa urahisi kwa lengo la ukaguzi wa Usalama na Afya Kazini na kufanya tathmini ya madhara yanayoweza kutokea ili kuweka mbinu za kukabiliana nayo.

16. Imetoa mafunzo maalum ya utoaji wa Huduma ya Kwanza kwa wafanyakazi 42 wa sekta binafsi, mafunzo ya Mwakilishi wa Usalama na Afya Kazini kwa wafanyakazi 100 (50 Umma, 50 Binafsi) na mafunzo ya Msingi wa Usalama na Afya Kazini katika sehemu za kazi kwa taasisi 12 (7 Binafsi, 5 Umma) ambapo jumla ya waajiri na waajiriwa 968 walipatiwa mafunzo hayo ili kuweza kutekeleza masuala ya usalama na afya wakiwa kwenye sehemu zao za kazi.

17. Imefanya uchunguzi wa afya za wafanyakazi 171 (Wanawake 99, Wanaume 72) wa muda maalum kwa watumishi wa Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ili kujua hali zao kiafya sambamba na kushajihisha taasisi za Serikali na za binafsi kufanya uchunguzi wa afya wa muda maalumu kwa wafanyakazi wao.

18. Imefanya mapitio ya Sheria ya Usalama na Afya Kazini nambari 8 ya mwaka 2005 na kuandaa kanuni zinazohusiana na masuala ya usalama na afya kazini (Kanuni Kiongozi na ya Kuripoti Maradhi Kazini).

19. Imeshiriki mikutano ya Kitaifa inayohusiana na Mashirikiano juu ya masuala ya Usalama na Afya Kazini na ya Kazi Dar es Salaam na Dodoma. **Kiambatisho namba 4 kinafafanua.**

**Programu Kuu: Programu Kuu ya Kukuza na Kuimarisha Uwekezaji Nchini**

**24. Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu Ndogo ya Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma kupitia Ushirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP), kwa mwaka wa fedha 2025/2026, imetekeleza shughuli zifuatazo;

1. Imefanya mapitio ya maandiko ya miradi (unsolicted proposals) 22 iliyowasilishwa na Sekta Binafsi ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Kati ya miradi 22 iliyopendekezwa na Sekta Binafsi, Miradi 6 kwenye Sekta ya uchukuzi. michezo na utalii imefikia hatua ya kusainiwa mikataba na kuanza utekelezaji.

2. Imefanya ufuatiliaji na Tathmini ya miradi 13 kati ya miradi 20 ya PPP kwa lengo la kutathmini utekelezaji wake. Tathmini imeonesha miradi ya umma iliyosainiwa mikataba ya PPP imeanza kutekelezwa kwa hatua mbalimbali ikiwemo ujenzi na kutoa huduma ikiwemo Bandari ya Fumba, Bandari ya Malindi na Kituo cha Ukaguzi wa vyombo vya moto-KwaSilva, Dole.

3. Imetoa mafunzo juu ya dhana na utaratibu wa utekelezaji wa miradi ya Umma inayotekelezwa kwa mfumo wa PP kwa taasisi za Umma ikiwemo Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara maalum za SMZ, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo. **Kiambatisho namba 5 kinafafanua.**

## D. UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA JULAI 2025 - MACHI 2026

**25. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Kukuza na Kuimarisha Uwekezaji Nchini pia inatekelezwa na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) ambapo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ilikusanya jumla ya TZS 4,886,000,085.33 sawa na asilimia 128 ya makadirio ya TZS 3,830,790,616 kutoka vyanzo vyake vya mapato. Aidha, ZIPA imetumia Jumla ya TZS 3,829,564,131.32 sawa na asilimia 99.9 ya makadirio ya matumizi.

**26. Mheshimiwa Spika,** kupitia Mamlaka imetekeleza Shughuli zifuatazo:-

1. Imesajili miradi ya uwekezaji 92 yenye thamani ya dola za kimarekani 561 Milioni kati ya Miradi 90 iliyokadiriwa kwa thamani ya Dola 390.67 Milioni katika sekta ya Utalii, Real estate, Viwanda na Mifugo.
2. Imeshiriki na kuandaa Mikutano 12, Makongamano 8 na Maonesho 4 ya kitaifa na kimataifa kwa lengo la kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini.
3. Kuendeleza ujenzi wa miundombinu katika maeneo huru ya uwekezaji ambapo ujenzi wa kilomita 8 za Barabara za ndani katika eneo la Fumba umeanza.
4. Mamlaka imefanya zoezi la ukaguzi na tathmini na ulipaji fidia katika maeneo makuu matano (5) ambayo ni eneo la ujenzi wa km 8 za barabara za ndani katika eneo la Uwekezaji Fumba, eneo la mradi wa IIT Madrasa, eneo la ujenzi wa AFCON,eneo la ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano ya Kimataifa na eneo la Dimani-Ndambani . Aidha Jumla ya TZS 175.9 milioni zimelipwa kwa ajili ya fidia katika eneo la AFCON (ICT Park).Vile vile jumla ya TZS 5.872 bilioni zinahitajika kulipwa kwa wananchi watakaoathirika na Miradi ya Uwekezaji.
5. Imekamilisha uandaaji wa ripoti ya awamu ya 17 ya utafiti wa mwenendo wa mitaji binafsi (Private Capital Flows - PCF).
6. Imesimamia utekelezaji wa Miradi ya Uwekezaji katika visiwa vidogovidogo ambapo visiwa 9 vimeshawekezwa.

7. Imekamilisha uandaaji wa Mpango Mkakati wa Uenezi na Masoko, Mkakati wa Mahitaji na matumizi ya mifumo ya kielektroniki na Mkakati wa Biashara na Uwekezaji wa Taasisi.
8. Imeimarisha huduma za Ofisi za Uwekezaji ikiwemo mifumo ya kielektroniki kwa kuunganisha mamlaka zote za kituo jumuishi (One Stop Centre), imetoa mafunzo kwa wafanyakazi na wadau na ununuzi wa Vitendea kazi.
9. Imeendelea na ujenzi wa Ofisi ya ZIPA katika eneo la Matrekta Mbweni Unguja kwa kujenga ukuta ili kudhibiti eneo la Ofisi.

## E. MWELEKEO WA UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE VYA MATUMIZI KWA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

### i Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA)

27. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) inatarajia kukusanya jumla ya TZS4.9 bilioni kutoka vyanzo vyake vya mapato. Aidha, ZIPA inatarajia kutumia Jumla ya TZS 4.09 bilioni kwa ajili ya Kazi za kawaida.

28. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka kwa mwaka 2026/2027 imepanga kutekeleza Shughuli zifuatazo:-

    1. Kufanya ziara za kimataifa za kuhamasisha uwekezaji kwa lengo la kuvutia wawekezaji wa kimkakati kuja Nchini Kuimarisha miundombinu ya barabara katika maeneo Huru ya Uchumi Fumba na Kuendeleza miundombinu ya usambazaji wa umeme na maji ndani ya Block “A” ya Eneo Maalumu la Kiuchumi Micheweni- Pemba.
    2. Kuaanda Mpango wa matumizi ya ardhi (Land Master Plan) katika eneo la Bandari Mangapwani na Block B katika eneo Huru la Uchumi Micheweni Pemba na upatikani wa hati milki kwa Maeneo Maalum ya Uchumi Pemba
    3. Kuaanda Mpango wa matumizi ya ardhi (Land Master Plan) katika eneo la Bandari Mangapwani na Block B katika Eneo Huru la Uchumi Micheweni Pemba na Upatikanaji wa hati za umiliki wa ardhi za mashamba ya Mpira Pemba.
    4. Kuandaa Mkutano wa Uwekezaji wa Zanzibar (Zanzibar Investment Summit) kwa ajili ya kuonesha fursa za uwekezaji na kukutanisha wadau kutoka ndani na nje ya Zanzibar.
    5. Kuwajengea uwezo watendaji wa mamlaka kwa lengo la kuongeza ufanisi na kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi na wawekezaji.
    6. Kuwawezesha wajumbe wa Zanzibar wanaoshiriki katika timu za majadiliano kati ya Tanzania Bara na nchi nyingine kuhusu masuala ya uwekezaji kwa kuwajengea uwezo wa kitaalamu, kiufundi na

kimajadiliano ili waweze kukidhi vigezo, kutetea maslahi ya Zanzibar kwa ufanisi, na kushiriki kikamilifu katika maandalizi, majadiliano na utekelezaji wa mikataba ya kimataifa ya uwekezaji (Bilateral Investment Treaties -BIT).

7. Kukamilisha Mkakati wa Uhamasishaji, Masoko na Mawasiliano (Promotion, Marketing and Communication - PMC) ili kuimarisha uhamasishaji na taswira ya Uwekezaji.
8. Kukamilisha uandaaji wa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Mamlaka.
9. Kuhamasisha na kutetea uanzishwaji wa vivutio vipya vya uwekezaji vinavyolenga sekta maalum ikiwemo Afya, Anga, TEHAMA, Usafirishaji Baharini Viwanda,
10. Kufanya tathmini ya thamani ya mali (property valuation) ndani ya Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZs) kwa ajili ya kuainisha fidia stahiki.
11. Kujenga maghala mapya 14 ndani ya Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZs), hususan katika eneo la Amani na Micheweni.
12. Kukamilisha awamu ya mwisho ya mfumo wa kielektroniki wa kuwahudumia wawekezaji (ZIEW) na mifumo mengine midogo ya ndani ili kuboresha utoaji wa huduma na kuongeza ufanisi wa taasisi.
13. Kujenga Ofisi mpya za Mamlaka ya Kukuza Uwekezaqji katika maeneo ya Micheweni kwa Pemba na Mbweni kwa Unguja,

**ii Kampuni ya Uwekezaji ya Zanzibar ( Zanzibar Investment Company Limited)**

**34. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeanzisha Kampuni maalumu ya Uwekezaji kwa lengo la kuongeza wigo kwa wawekezaji ambao wanania ya kuwekeza kwa utaratibu wa hisa kwa kushirikiana na Serikali. Kwa mwaka 2026/2027 kampuni imepangiwa kutumia Jumla ya TZS 350,000,000 na itatekeleza shughuli zifuatazo:-

1. Kukamilisha muundo wa Kampuni kwa ajili ya uongozi, usimamizi na kuweka utaratibu wa kazi, na uwajibikaji.
2. Kutafuta Jengo, Ununuzi wa Samani na Vifaa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Kampuni.
3. Kuandaa Mpango Mkakati wa miaka mitatu kwa ajili ya kuweka malengo mahsusi ya muda mfupi na mrefu ya Kampuni ikiwemo mpango wa biashara na upatikanaji wa mtaji.
4. Kuanza mchakato wa upatikanaji wafanyakazi na kuwajengea uwezo.
5. Kujenga uelewa kwa wadau wa ndani na nje, na kutangaza fursa za uwekezaji kupitia hisa za Kampuni.
6. Kuishauri Serikali maeneo sahihi ya uwekezaji kupitia tafiti na uchambuzi wa soko na taarifa za kiuwekezaji.

## F. MWELEKEO WA VIPAUMBELE VYA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

### i. Programu za Wizara ya Kazi na Uwekezaji

### Programu Kuu: Uendeshaji na Uratibu wa Wizara

35. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027, imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo;

1. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Bajeti, Mipango pamoja na Miradi ya Maendeleo ya Wizara.
2. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mpango Mkakati, Programu na Miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara.
3. Kuratibu Uandaaji wa Sera ya Kazi na Mapitio ya Sera ya PPP, Sheria na Miongozo zinazohusu shughuli zinazotekelezwa na Wizara.
4. Kuratibu na kuandaa Vikao vya Mashirikiano Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.
5. Kuratibu na kusimamia Tafiti zinazofanywa na Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara.
6. Kufanya Mapitio ya Nyenzo za Kukusanyia Takwimu za Wizara na uaandaji Muhtasari wa Takwimu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS).
7. Kuendelea kuwapatia Watumishi Stahiki zao ikiwemo Mishahara, Maposho (Likizo, Safari) na Muda wa ziada (Overtime) pamoja na malipo ya Ubani kwa Wafiwa.
8. Kuwapatia Wafanyakazi Mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa mujibu ya Miongozo ya Utumishi wa Umma pamoja na kuwapima utendaji kazi.
9. Kuhakikisha uwepo kwa Vitendea kazi vya kutosha pamoja na mazingira bora ya kazi .
10. Kuimarisha Mifumo ya TEHAMA na Habari na Mawasiliano.

11. Kuimarisha Mifumo ya Ulinzi kwa kuweka Security Fence na CCTV Camera pamoja na kuhakikisha Wafanyakazi wanapata vitambulisho vya Ofisi.

12. Kutoa huduma za kiutawala na kiuendeshaji

13. Kuratibu shughuli za Ofisi Pemba kwa kusimamia utekelezaji wa masuala ya kazi na mahusiano kazini, utatuzi wa migogoro ya kazi, Usalama na Afya Kazini uwekezaji binafsi na Uwekezaji wa Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, utumishi, uendeshaji na mipango ya Wizara.

**36.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara inaliomba Baraza lako kuidhinisha TZS 4,625,669,000 (TZS 1,094,138,000 kwa Programu Ndogo ya Uratibu wa Ofisi Pemba na TZS 3,531,531,000 kwa uratibu wa shughuli Unguja ) kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kazi na Uwekezaji.

**Programu Kuu ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi na Upatikanaji wa Ajira**

**37.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027, imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo;

1. Kuimarisha sheria za kazi kwa kufanya ukaguzi kazi kwa Taasisi Binafsi 720 Unguja na Pemba pamoja na ukaguzi wa vyama vya wafanyakazi
   8 na jumuiya 2 za waajiri kwa lengo la kuhakikisha utekelezaji wa sheria za kazi.

2. Kusuluhisha na kuamua migogoro inayohusiana na masuala ya kazi na ya vyama vya wafanyakazi na Jumuiya za Waajiri ili kuwepo na mahusiano bora mahala pa kazi.

3. Kuthibitisha mikataba ya kazi 12,000 ya wafanyakazi wa ndani na wa nje ya nchi kwa lengo la kuhakikisha mikataba hiyo inakidhi viwango vya kazi Kimataifa.

4. Kuendelea na hatua za kuridhia mikataba sita ya Shirika la Kazi Duniani inayohusiana na Hifadhi ya jamii, wafanyakazi wa majumbani, usalama na afya kazini, mafao ya wafanyakazi wanaopata majanga

kazini, sera ya ajira na mfumo wa uhamasishaji wa masuala ya usalama na afya kazini.

5. Kuendelea kusimamia utoaji vibali vya kazi kidigitali kwa raia wa kigeni wanaokuja kufanya kazi Nchini.
6. Kuendelea kufanya tathmini za viwango vya mshahara mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa maslahi ya wafanyakazi yanaendana na hali halisi ya uchumi na mahitaji ya wananchi.
7. Kupambana na ajira za watoto katika sehemu za kazi kwa ajili ya kuzuia utumikishwaji wa Watoto chini ya miaka 18.
8. Kukamilisha sheria za kazi ili ziendane na mabadiliko ya wakati uliopo, hali ya uchumi pamoja na kulinda maslahi ya wafanyakazi na waajiri.
9. Kuendelea na hatua za uanzishwaji wa programu za mafunzo ya kazi na mahusiano kazini (labour relations training program).
10. Kutoa elimu kwa waajiri, waajiriwa na jamii katika masuala ya kazi ili kuongeza uelewa wa Sheria za kazi, miongozo pamoja na haki na wajibu katika maeneo ya kazi.
11. Kuendelea na mfumo wa usimamizi wa taarifa za kazi kidijitali (comprehensive labour management system) ili kuimarisha taarifa za kazi.
12. Kukuza na kuimarisha mashirikiano ya UTATU baina ya Serikali, Vyama vya wafanyakazi na Jumuiya ya waajiri ili kuondosha changamoto za kazi.
13. Kuwawezesha wajumbe wa Zanzibar wanaoshiriki katika timu ya Majadiliano kati ya Tanzania na Nchi nyingine kuhusu masuala ya kazi kwa kuwajengea uwezo wa kitaalamu, kiufundi na kimajadiliano ili waweze kukidhi vigezo, kutetea maslahi ya Zanzibar kwa ufanisi, na kushiriki katika maandalizi, majadiliano na utekelezaji wa mikataba ya kimataifa ya kazi (Bilateral Labour Agreements - BLA).

14. Kukagua sehemu za kazi 400 na kusajili sehemu 200 za kazi kwa lengo la kulinda usalama na afya kazini

15. Kuandaa mfumo wa kielektoniki (Workplace Information Management System (WIMS)) wa usimamizi wa Usalama na Afya Kazini

16. Kusimamia Sheria ya Usalama na Afya kazini na kuanda kanuni 7 zinazohusiana na masuala ya Usalama na Afya Kazini

17. Kushiriki mikutano na makongamano ya kitaifa na kimataifa yanayohusiana na masuala ya Usalama na Afya Kazini

18. Kutoa elimu kwa wajiri, wajiriwa na jamii katika masuala ya kazi, vyama vya wafanyakazi na Usalama na Afya Kazini.

38. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara inaliomba Baraza lako kuidhinisha TZS 2,791,710,000 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Programu ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi na Upatikanaji wa Ajira.

**Programu Kuu: Kukuza na Kuimarisha Uwekezaji Nchini**

39. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027, imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo;

1. Kufanya Mapitio ya Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo ya PPP ili iendane na mabadiliko ya wakati na mazingira ya sasa ya Zanzibar kiuchumi kwa lengo kulinda maslahi ya Zanzibar, kuimarisha utekelezaji wa miradi ya PPP iliyopo na kuvutia wawekezaji zaidi.

2. Kuratibu uwekezaji wa Miradi ya Umma inayotekelezwa kwa mfumo wa PPP inayoanzishwa na Sekta Binafsi (Unsolicited PPP Projects) kwa kuzingatia mitaji, Teknolojia, Ubunifu na njia mpya za Utekelezaji.

3. Kuratibu uwekezaji wa Miradi ya Umma inayotekelezwa kwa mfumo wa PPP inayoanzishwa na Sekta Umma (Solicited PPP Projects) kwa kuzingatia masharti na mahitaji ya Serikali.

4. Kuanzisha Kanzi Data ya Upembuzi Yakinifu kwa miradi inayotarajiwa kutekelezwa na inayotekelezwa kwa mfumo wa PPP kwa lengo la kuhifadhi na kuratibu taarifa zote sehemu mmoja ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa.
5. Kuendelea kuwajengea Uwezo, kupitia mafunzo maalumu ya kitaaluma na mafunzo kazini watendaji wa Idara kwa lengo la kuelewa vyema Sheria, taratibu na mbinu za kusimamia Miradi ya Umma inayotekelezwa kwa mfumo wa PPP.
6. Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi 16 ya Umma inayotekelezwa kwa mfumo wa PPP kwa lengo la na kubaini ufanisi wa utekelezaji, matokeo yaliyopatikanana changamoto zilizopo.
7. Kuendelea kuwajengea uwezo wa kitaalamu watendaji wa Serikali kupitia Mawizara, Idara na Taasisi wa kuandaa miradi ya umma itakayotekelezwa kwa mfumo wa PPP kwa lengo la kuhakikisha uwazi, ufanisi na kulinda maslahi ya serikali, wawekezaji na wananchi.
8. Kuandaa na kushiriki semina na warsha za PPP na mikutano ya majadiliano na wadau kutoka Sekta Binafsi, Sekta za Umma, Wafadhili na Taasisi za kifedha na wananchi kwa ujumla ili kuongeza uelewa na kuondoa hofu na upotoshaji wa taarifa za uwekezaji kupitia miradi ya Umma inayotekelezwa kwa mfumo wa PPP.

**40. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara inaliomba Baraza lako kuidhinisha TZS 19,674,201,000 Kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Programu ya Kukuza na Kuimarisha Uwekezaji Nchini.

### ii Uzingatiaji wa Usawa wa Kijinsia

**41. Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2026/2027 utazingatia Jinsia kwa kuwashirikisha Vijana, Wanawake na makundi maalum katika kusimamia na kutekeleza masuala ya kazi na mahusiano ya kazi, Usalama na Afya Kazini na katika Uwekezaji Binafsi na Uwekezaji wa Ushirikiano baina ya Sekta za Umma na Sekta Binafsi .

### iii. Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara.

42. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kazi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS. 8,500,000,000** kupitia vianzio vyake Vinne (4) ambavyo ni Ada ya Usajili, Ada za Mikataba, Ada za Vibali vya kazi kwa Wasio Raia na Ada za Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi. Kiambatisho nambari 6 Kinafafanua.

43. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara ya Kazi na Uwekezaji imekadiriwa matumizi ya jumla ya TZS. 27,091,580,000 Kati ya fedha hizo TZS. 6,873,280,000 ni Mishahara; TZS. 5,218,300,000 ni kwaajili ya Matumizi ya Kawaida; TZS 15,000,000,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. **Kiambatanisho nambari 7a kinafafanua.**

## SHUKURANI NA HITIMISHO

44. **Mheshimiwa Spika,** Nahitimisha hotuba hii kwa mara nyengine kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuwaendelea kuiweka Nchi yetu katika hali ya amani na utulivu, na tunamuomba kwa rehema zake azidi kutujaalia kudumu kwa amani hiyo. Aidha, napenda kutoa shukurani na pongezi za dhati kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, na Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuendelea kuiongoza Nchi yetu kwa umahiri mkubwa na kusimamia misingi ya haki, demokrasia na utawala bora. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awaongezee viongozi wetu hawa hekima, busara, afya njema na nguvu katika kuendelea kuliongoza Taifa letu kuelekea maendeleo na ustawi wa wananchi wake.

45. **Mheshimiwa Spika,** Nawashukuru na kuwapongeza Watendaji na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Kazi na Uwekezaji, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Khamis Suleiman Mwalim Shibu, pamoja na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Rashid Ali Salim, kwa kujituma kwao na kuendelea kusimamia kwa ufanisi utekelezaji wa majukumu, mipango na shughuli mbalimbali za Wizara. Aidha, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Afisa Mdhamini Pemba; Mkurugenzi Mtendaji ZIPA, Kamishna wa Kazi, Kamishna wa PPP, na Wakurugenzi wa Idara ya Usalama na Afya Kazini na Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Natoa pongezi na shukurani za dhati kwa Ndugu Bihindi Nassor Khatib aliyekuwa Mkurugenzi wa Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ambaye amestaafu kwa mchango wake mkubwa alioutoa katika kufanikisha Maendeleo ya Wizara. Aidha nawashkuru Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi zilizopo chini ya Wizara,Wakuu wa Divisheni na Vitengo, pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa kwa ushirikiano wao mzuri, uwajibikaji na juhudi wanazoendelea kuzionesha katika kuhakikisha Wizara inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa manufaa ya Taifa na wananchi kwa ujumla.

46. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kazi na Uwekezaji inatanguliza shukurani zake za dhati kwa ushirikiano mzuri kupitia taasisi tunazofanyakazi nao pamoja, zikiwemo Wizara, Taasisi za Serikali, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Taasisi Binafsi, Washirika wa Maendeleo, Mabenki, Asasi za Kiraia na Jamii kwa ujumla. Wizara inawashukuru Washirika wa Maendeleo tunaofanyakazi nao ambao ni ILO, UNDP, FAO, IOM, Benki ya Dunia (World Bank) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Mendeleo Kusini mwa Afrika. Aidha, Wizara inazishukuru Taasisi za Kiraia zikiwemo ZATUC, ZANEMA, Mawakala Binafsi wa Ajira, Zanzibar na Taasisi zote zinazoshirikiana nazo kwani si rahisi kuzitaja moja moja. Wizara pia inazishukuru Benki ya PBZ, BOT, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA), Polisi, Uhamiaji, Ustawi wa Jamii na Sekretarieti ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu.

47. **Mheshimiwa Spika**, Kwa niaba ya Wizara ya Kazi na Uwekezaji Zanzibar, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji, pamoja na Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Ajira na Mahusiano Kazini, ambao ni Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ushirikiano mzuri na wa karibu katika kusimamia na kuendeleza Sekta ya Kazi na Uwekezaji. Aidha, nawaomba tuendelee kuimarisha ushirikiano wetu kwa pamoja ili kuhakikisha wananchi na wadau wa Sekta ya Kazi na Uwekezaji wanaendelea kupatiwa huduma bora, zenye ufanisi na tija kwa maendeleo ya Taifa letu.

48. **Mheshimiwa Spika,** Natoa shukurani za dhati kwa Uongozi wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa msaada na ushirikiano mkubwa katika kuwezesha uwekaji lami sehemu ya Ndani na sehemu ya Nje ya Wizara yetu. Hatua hii imechangia kuimarisha mazingira ya kazi, kurahisisha usafiri na mawasiliano, pamoja na kuongeza hadhi na usalama kwa eneo la Wizara. Aidha, tuna imani kuwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi itakamilisha mahitaji yetu mengine yaliyobaki ya kuimarisha miundombinu ya Wizara, katika mwaka wa fedha 2026/2027.

49. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kutoa shukrani za dhati kwa Shirika la Kazi Duniani ILO (International Labour Organization, chini ya uongozi mahiri wa Bi. Caroline Khamati Mugalla, Mkurugenzi Mkaazi wa ILO Kanda ya Afrika Mashariki, kwa ushirikiano na msaada wa kitaalamu pamoja na kifedha wanaoendelea kuipatia Zanzibar katika maendeleo ya Sekta ya Kazi. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, kwa kushirikiana na ILO na wadau wa Sekta ya Kazi, tumefanikiwa kuandaa Mpango wa Taifa wa Kazi Zenye Staha Awamu ya Tatu (2025/2026–2029/2030), kuoanisha sheria za kazi na Viwango vya Kazi vya Kimataifa, pamoja na kuandaa rasimu ya Mpango wa Taifa wa Kupinga Ajira kwa Watoto (2026–2032). Tutaendelea kushirikiana kwa karibu na Shirika la Kazi Duniani (ILO) katika kuimarisha maendeleo ya Sekta ya Kazi na ukuaji wa uchumi wetu.

50. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati Ndugu Khamis Mwinyi Mohammed, Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Zanzibar, Zanzibar Trade Union Congress (ZATUC) na Ndugu Salahi Salim Salah, Mkurugenzi Mtendaji wa Jumuiya ya Waajiri Zanzibar, Zanzibar Employers Association (ZANEMA), kwa mchango wao mkubwa sana katika maendeleo ya Sekta ya Kazi nchini. Viongozi na wanachama wa ZATUC na ZANEMA wameendelea kushirikiana kwa karibu na Serikali kupitia Wizara ya Kazi, katika kuimarisha mahusiano ya kikazi, kulinda haki za wafanyakazi na waajiri, pamoja na kutatua changamoto za masuala ya kazi, kwa njia ya majadiliano na maridhiano, na hivyo kuchangia kudumisha amani, utulivu na kukuza uchumi jumuishi. Tunawaomba tuendelee kushirikiana kwa karibu zaidi kwa maendeleo ya sekta ya kazi na taifa kwa ujumla.

51. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, navishukuru vyombo vyote vya habari vinavyoshirikiana nasi katika kuelemisha jamii juu ya shughuli zinazofanywa na Wizara. Vyombo hivyo vimechangiya kwa kiasi kikubwa shughuli za Wizara yetu kujulikana na jamii, Ndani na Nje ya Zanzibar. Nawashkuru wote wanaoshirikiana nasi katika kutekeleza majukumu yetu kwa njia moja au nyengine. Nawaomba waendelee kuwa nasi katika kufanikisha malengo ya kuwaletea wananchi maendeleo endelevu. Nawashkuru kwa dhati Wawekezaji wote waliowekeza na wale wote waliyoonesha nia ya kuja kuwekeza nchini. Aidha,tunawaomba Wadau wetu wote kuendelea kusaidia juhudi za serikali kuendeleza sekta za Kazi na Uwekezaji.

52. **Mheshimiwa Spika;** Nachukua fursa hii kuishukuru familia yangu hususan Mke wangu mpendwa na Watoto wangu kwa ushirikiano, Uvumilivu na Uelewa munaonionesha katika kutekeleza majukumu niliyopewa ya Kazi. Mchango wenu umekuwa chachu muhimu ya kunipa Utulivu, Moyo na Ari ya kuendelea kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi na kuwajibika ipasavyo katika nafasi niliyopewa. Nathamini sana namna ninavyoelewa ugumu wa kazi yangu na mnavyoniwezesha kupata utulivu katika kunitia moyo wakati wa changamoto. Bila ya mshikamano Uvumilivu na maombi yenu mambo mengi yasingewezekana.

53. **Mheshimiwa Spika;** Kwa unyenyekevu na heshima kubwa, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuniamini na kunipa dhamana ya kusimamia Sekta ya Kazi na Uwekezaji. Ninampongeza kwa Uongozi wake Mahiri, wenye hekima na juhudi zisizochoka katika kuwaletea maendeleo, amani na ustawi wananchi wa Zanzibar, kupitia maono yake thabiti na Sera zenye muelekeo wa kuimarisha Uchumi, Ustawi wa jamii na Usawa wa maendeleo katika kila Sekta, tumeshuhudia mafanikio makubwa ambayo yanagusa maisha ya watu wote kwa njia chanya. Naahidi nitafanya kazi kwa uadilifu na moyo wa kujitolea na kuendelea kumpa ushirikiano na kuunga mkono jitihada zake ili kuifikisha Nchi yetu katika mafanikio makubwa zaidi.

54. **Mheshimiwa Spika,** Aidha kwa dhati kabisa nakishukuru Chama changu, Chama Cha Mapinduzi,Viongozi na Wanachama wote kwa kuniamini na kunipa ushirikiano wa dhati na moyo wa mshikamano ulionisaidia kuweza kutekelezaji Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 kwa kishindo. Nawashukuru. Asanteni sana.

55. **Mheshimiwa Spika;** Baada ya kuwasilisha Hotuba hii, naomba tena kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako kwa ushirikiano wao wanaonipatia. Aidha, ninawaomba Wajumbe kuipokea Hotuba hii, kujadili na hatimae kuikubali taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026

na kuidhinisha makadirio ya Mapato Jumla ya **TZS. 8,500,000,000** na matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya jumla ya **TZS. 27,091,580,000** ili kufanikisha malengo tuliyojiwekea kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**56. Mheshimiwa Spika;** Naomba kutoa hoja.

…………………………………………..

**MHESHIMIWA SHARIFF ALI SHARIFF (MBM)**

**WAZIRI WA KAZI NA UWEKEZAJI**

## G. VIAMBATISHO

### Kiambatisho nambari 1

# MUHTASARI WA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

| KASMA NAMBA | IDARA | VYANZO VYA MAPATO | MAKADIRIO YA MWAKA | MAKADIRO YA MIEZI 9 | MAKUSANYO HALISI MIEZI 9 | % YA MAPATO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1422012 | KAMISHENI YA KAZI | UTHIBITISHO WA MIKATABA YA KAZI | 400,000,000 | 292,000,000.00 | 365,903,607 | 125 |
| 1422071 | IDARA YA USALAMA NA AFYA KAZINI | ADA YA UKAGUZI WA USALAMA NA AFYA MAENEO YA KAZI. | 1,169,695,917 | 852,271,937.00 | 246,790,000 | 29 |
| 1422075 | IDARA YA AJIRA | ADA YA UHAKIKI WA MIKATABA YA AJIRA | 270,000,000 | 204,000,000.00 | 133,660,000 | 66% |
| 1422036 | IDARA YA MAENDELEO YA USHIRIKA | ADA YA USAJILI YA WA VYAMA VYA USHIRIKA | 160,000,000 | 127,200,000.00 | 22,680,000 | 18% |
| 1422037 | IDARA YA MAENDELEO YA USHIRIKA | ADA YA UKAGUZI YA WA VYAMA VYA USHIRIKA | 120,000,000 | 88,450,000.00 | 16,065,000 | 18% |
| 1422011 | KAMISHENI YA KAZI | ADA YA VIBALI VYA KAZI KWA WAGENI | 4,739,391,808 | 3,304,492,356.00 | 3,975,789,600 | 120% |
| | **JUMLA NDOGO UNGUJA** | | **6,859,087,725.00** | **4,868,414,293.00** | **4,760,888,207** | 98% |
| 1422012 | KAMISHENI YA KAZI | UTHIBITISHO WA MIKATABA YA KAZI | 15,000,000 | 9,960,000.00 | 9,412,000 | 94% |

| KASMA NAMBA | IDARA | VYANZO VYA MAPATO | MAKADIRIO YA MWAKA | MAKADIRO YA MIEZI 9 | MAKUSANYO HALISI MIEZI 9 | % YA MAPATO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1422037 | IDARA YA MAENDELEO YA USHIRIKA | ADA YA UKAGUZI YA WA VYAMA VYA USHIRIKA | 42,000,000 | 32,100,000.00 | 2,890,000 | 9% |
| | JUMLA NDOGO PEMBA | | 350,000,000.00 | 256,710,000.00 | 58,245,000 | 23% |
| | JUMLA KUU | | 7,209,087,725.00 | 5,125,124,293.00 | 4,819,133,207 | 94% |

**Kiambatisho nambari 2a**

## MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

| PROGRAMU | JUMLA YA BAJETI (OC+SALARY+DEV) 2025/2026 | JUMLA YA MAKADIRIO YA OC + MSHAHARA +DEV.) JULAI -MACHI 2025/2026 | JUMLA YA MATUMIZI YA OC + MSHAHARA +DEV.) JULAI -MACHI 2025/2026 | % YA MAKADIRIO YA JULAI -MACHI 2025/2026 | % YA BAJETI YA MWAKA 2025/2026 |
|---|---|---|---|---|---|
| **P01 Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kazi na Uwekezaji** | 6,036,969,700 | 4,574,610,359 | 2,897,282,394 | 63 | 48 |
| S0101: Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti | 1,014,614,000 | 842,833,000 | 273,573,536 | 32 | 27 |
| S0102: Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji | 3,027,729,000 | 2,226,647,750 | 1,841,800,911 | 83 | 61 |
| S0103: Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba | 1,994,626,700 | 1,505,129,609 | 781,907,947 | 52 | 39 |
| **Programu Kuu ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi na Upatikanaji wa Ajira** | 2,082,670,300 | 1,586,039,197 | 958,504,421 | 60 | 46 |
| S0201: Programu Ndogo ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi na Usuluhishi wa Migogogro ya Kazi | 1,781,924,300 | 1,308,223,197 | 913,604,421 | 70 | 51 |
| S0202: Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini | 300,746,000 | 277,816,000 | 44,900,000 | 16 | 15 |

| PROGRAMU | JUMLA YA BAJETI (OC+SALARY+DEV) 2025/2026 | JUMLA YA MAKADIRIO YA OC + MSHAHARA +DEV.) JULAI -MACHI 2025/2026 | JUMLA YA MATUMIZI YA OC + MSHAHARA +DEV.) JULAI -MACHI 2025/2026 | % YA MAKADIRIO YA JULAI -MACHI 2025/2026 | % YA BAJETI YA MWAKA 2025/2026 |
|---|---|---|---|---|---|
| **P03: Programu Kuu ya Kukuza na Kuimarisha Uwekezaji Nchini** | 19,630,645,000 | 14,719,149,250 | 6,225,290,866 | 42 | 32 |
| S0301: Programu Ndogo ya Usimamizi wa Uwekezaji Binafsi | 18,911,300,000 | 14,183,475,000 | 6,063,358,891 | 43 | 32 |
| S0302:Programu Ndogo ya Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma kupitia Ushirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) | 719,345,000 | 535,674,250 | 161,931,975 | 30 | 23 |
| JUMLA KUU | 27,750,285,000 | 20,879,798,806 | 10,081,077,681 | 48 | 36 |

**Kiambatisho nambari 2b**

## MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

| Maelezo | Mapato | Matumizi |
|---|---|---|
| Lengo la mwaka | 7,209,087,725 | 27,750,285,000 |
| Makadirio miezi 9 | 5,125,124,293 | 20,879,798,806 |
| Fedha zilizopatikana | 4,819,133,207 | 10,081,077,681 |
| Asilimia ya Makadirio | 94% | 48% |
| Asilimia ya mwaka | 72% | 36% |

**Kiambatisho nambari 3**

## PROGRAM ZA WIZARA YA KAZI NA UWEKEZAJI

| | |
|---|---|
| **P01** | **Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kazi na Uwekezaji** |
| S0101 | Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti |
| S0102 | Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji |
| S0103 | Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba |
| **P02** | **Programu Kuu ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi na Upatikanaji wa Ajira** |
| S0201 | Programu Ndogo ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi na Usuluhishi wa Migogogro ya Kazi |
| S0202 | Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini |
| **P03** | **Programu Kuu ya Kukuza na Kuimarisha Uwekezaji Nchini** |
| S0301 | Programu Ndogo ya Usimamizi wa Uwekezaji Binafsi |
| S0302 | Programu Ndogo ya Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma kupitia Ushirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) |

**Kiambatisho nambari 4**

## UTEKELEZAJI WA PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA VIWANGO VYA KAZI NA UPATIKANAJI WA AJIRA KWA KIPINDI CHA JULAI

| S/N | SHUGHULI | LENGO | UTEKELEZAJI | % |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ukaguzi Kazi | 708 | 326 | 46 |
| 2 | Uthibitishwaji wa Mikataba ya Kazi | 10,500 | 11,613 | 111 |
| 3 | Vibali vya Wageni | 3,430 | 2,877 | 84 |
| 4 | Upokeaji wa Migogoro ya Kazi | 200 | 295 | 148 |
| 5 | Kuondoa watoto chini ya miaka 18 katika Ajira za kutumikishwa | 1,000 | 1,178 | 118 |
| 6 | Ukaguzi wa Usalama na Afya Kazini | 240 | 365 | 152 |
| 7 | Usajili wa sehemu za kazi kwa ajili ya kuangalia masuala ya Usalama na Asfya Kazini | 120 | 119 | 99 |

**Kiambatisho nambari 5**

## UTEKELEZAJI WA PROGRAMU KUU YA KUKUZA NA KUIMARISHA UWEKEZAJI NCHINI

| S/N | SHUGHULI | LENGO | UTEKELEZAJI | % |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Usajili wa miradi ya PPP | 20 | 6 | 30 |
| 2 | Mapitio ya Maandiko ya Miradi (fs) ya PPP | 22 | 22 | 100 |
| 3 | Ukaguzi na Ufatiliaji wa Miradi ya PPP | 20 | 13 | 65 |
| 4 | Usajili wa Miradi ya Uwekezaji (ZIPA) | 90 | 92 | 102 |
| 5 | Kuekeza Mtaji wa Miradi | USD 390.7 | USD 561 | 144 |
| 6 | Ukasanyaji wa Mapato | 3,830.8 | 4,886 | 128 |

**Kiambatisho nambari 6**

## Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

| Na | Vyanzo vya makusanyo "000" | Unguja | Pemba |
|---|---|---|---|
| 1 | Ada ya Usajili | 379,000 | - |
| 2 | Ada ya Mikataba | 586,000 | 256,500 |
| 3 | Ada ya vibali vya Kazi kwa Wasio Raia | 5,090,000 | 292,700 |
| 4 | Ada za Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi | 1,594,500 | 300,000 |
| Jumla Unguja na Pemba | | 7,650,000 | 850,000 |
| **Jumla Kuu** | | | **8,500,000** |

**Kiambatisho nambari 7a**

## MAOMBI YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2026/2027

| PROGRAMU | MATUMIZI YA KAWAIDA | MISHAHARA | RUZUKU YA OC | RUZUKU YA MISHAHARA | MAENDELEO | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **P01 Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kazi na Uwekezaji** | **2,506,292** | **2,119,377** | - | - | - | **4,625,669** |
| S0101: Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti | 638,154 | 222,212 | | | | **860,366** |
| S0102: Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji | 1,296,850 | 1,374,315 | | | | **2,671,165** |
| S0103: Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba | 571,288 | 522,850 | | | | **1,094,138** |
| **Programu Kuu ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi na Upatikanaji wa Ajira** | - | - | **1,689,080** | **1,102,630** | - | **2,791,710** |
| S0201: Programu Ndogo ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi na Usuluhishi wa Migogogro ya Kazi | | | 1,089,080 | 1,102,630 | | **2,191,710** |
| S0202: Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini | | | 600,000 | | | **600,000** |
| **P03: Programu Kuu ya Kukuza na Kuimarisha Uwekezaji Nchini** | **1,022,928** | **86,403** | - | **3,564,870** | **15,000,000** | **19,674,201** |
| S0301: Programu Ndogo ya Usimamizi wa Uwekezaji Binafsi | | | | 3,564,870 | 15,000,000 | **18,564,870** |

| PROGRAMU | MATUMIZI YA KAWAIDA | MISHAHARA | RUZUKU YA OC | RUZUKU YA MISHAHARA | MAENDELEO | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| S0301: Programu Ndogo ya Usimamizi wa Uwekezaji Binafsi | | | | 3,564,870 | 15,000,000 | **18,564,870** |
| S0302:Programu Ndogo ya Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma kupitia Ushirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) | 672,928 | 86,403 | | | | **759,331** |
| Kusimamia Uwekezaji kupitia hisa za Kampuni ya Serikali | 350,000 | | | | | |
| JUMLA KUU | **3,529,220** | **2,205,780** | **1,689,080** | **4,667,500** | **15,000,000** | **27,091,580** |

**Kiambatisho nambari 7b**

## MAOMBI YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2026/2027

| Maelezo | Mapato | Matumizi | Asilimia ya Matumizi |
|---|---|---|---|
| Jumla | 8,500,000,000 | 27,091,580,000 | 100% |
| Mshahara | - | 6,873,280,000 | 25% |
| Matumizi ya Kawaida | - | 5,218,300,000 | 19.2% |
| Miradi ya Maendeleo | - | 15,000,000,000 | 55.3% |